KATIBA YA CHAMA

CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA AFYA TANZANIA

(TUGHE)

1994 NA MAREKEBISHO YA KATIBA TOLEO LA TANO MWAKA 2019

CHAMA HIKI KIMEUNDWA CHINI YA SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO KAZINI SURA 366 MAREJEO YA 2019

KATIBA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA AFYA TANZANIA

TANZANIA UNION OF GOVERNMENT AND HEALTH EMPLOYEES (TUGHE)

CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA AFYA TANZANIA

TANZANIA UNION OF GOVERNMENT AND HEALTH EMPLOYEES (TUGHE)

BARABARA YA JAKAYA KIKWETE
KIWANJA NA. 5
Block Na. G,
MJI WA DODOMA

S.L.P. 2364

DODOMA

SIMU: 026 232 4520

NUKUSHI: +255 26 232 4520

BARUA PEPE: info@tughe.or.tz

YALIYOMO

JINA ..... **(i)**

ANUANI YA CHAMA ..... **(ii)**

YALIYOMO ..... **(iii)**

UTANGULIZI, TAMKO, KAULI NA FASILI..... **(iv)**

Sura ya Kwanza **MISINGI YA CHAMA** **1**

Sura ya Pili **MADHUMUNI YA CHAMA**..... **3**

Sura ya Tatu **UANACHAMA**..... **8**

Sura ya Nne **OFISI ZA CHAMA**..... **18**

Sura ya Tano **VIONGOZI NA MAOFISA WAKUU WA CHAMA**..... **20**

Sura ya Sita **VIKAO VYA CHAMA**..... **33**

Sura ya Saba **BARAZA LA WADHAMINI**..... **66**

Sura ya Nane **MIGOGORO YA KIKAZI**..... **70**

Sura ya Tisa **MAPATO YA CHAMA**..... **72**

Sura ya Kumi **MENGINEYO**..... **76**

UTANGULIZI:

A (i) Kwa kuwa sisi Wafanyakazi wa Serikali na Afya wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, kazi yetu kubwa ni kutoa huduma kwa Watanzania wote, huduma iliyotukuka na bora kwa Jamii yote, kwa pamoja Watumishi wa Serikali na Afya, Sekta hizi tumeazimia kuungana na kuunda Chama chetu, kitakachotuunganisha na kuhakikisha kuwa tunatekeleza wajibu wetu na baada ya kutekeleza wajibu wetu tupate haki zote zinazostahili kutoka kwa Waajiri wetu; Kama Raia wengine wote Nchini. Sisi Wafanyakazi tuna haki ya kupata huduma bora za Kijamii, Kiuchumi, Kimaslahi, Afya, Elimu Chakula, Maji, Malazi, Usafiri na huduma zingine zote zinazostahili.

(ii) Hivyo hatuna Chama kingine tena baada ya kuundwa Chama hiki na kwa hiari yetu, tunaamua pia kujishirikisha na Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania tunaazimia kuwa Wanachama wa TUCTA.
Kwa misingi hiyo sisi Wafanyakazi wa Serikali na Afya tunaanzisha Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania. 'Tanzania Union of Government and Health Employees (TUGHE) na kuipitisha rasmi Katiba ya CHAMA na kuamua kutumika mara moja.

(iii) Katiba hii itaitwa "KATIBA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA AFYA TANZANIA", kwa kifupi TUGHE na kwa Kiingereza "THE CONSTITUTION FOR TANZANIA UNION OF GOVERNMENT AND HEALTH EMPLOYEES", (TUGHE)

B. **"Huduma bora Maslani zaidi".**

C. Mahali popote katika Katiba hii isipokuwa kama maelezo yatafafanua vinginevyo:-

(i) **Mfanyakazi**:- Ina maana ya mtu aliyeingia katika makubaliano au Mkataba wa maandishi na Mwajiri yeyote yule kwa kufanya kazi kupewa Fidia/Malipo ya Ujira au Mshahara kwa mwezi au muda maalum na Mwajiri huyo.

(ii) **Wadhamini:**- Ina maana ya Wasimamizi wa Mali za Chama walio-chaguliwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(iii) **Mwanachama:**- Ina maana ya Mfanyakazi ambaye amekubali kujiunga na Chama hiki na ambaye ametoa/ atatoa michango yake ya kila mwezi katika Chama hiki.

(iv) **Baraza la Wadhamini:**- Ina maana Chombo cha Wadhamini wa Chama chenye Wajumbe wasiozidi wanne.

(v) ***Chama*:**- Ina maana Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) au Tanzania Union of Government and Health Employees TUGHE.

(vi) **Kanuni:**- Ina maana ya kanuni zilizotungwa kwa mujibu wa Katiba hii

(vii) **Katiba:**- Ina maana ya katiba ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE)

(viii) **Watendaji:**- Ina maana ya Watumishi walioteuliwa na kuajiriwa na Chama kwa Mkataba maalumu au Mkataba wa Kudumu.

(ix) **Kiongozi:**- Ina maana ya Mwanachama yeyote aliyechaguliwa na Chama au Kuteuliwa au Kuajiriwa na Chama kushika nafasi yoyote ya Uongozi katika Chama.

(x) **Katibu Mkuu:**- Ina maana Mtendaji Mkuu wa Chama ambaye ameidhinishwa kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Katiba hii.

(xi) **Makubaliano au Mkataba:**- Ina maana ya maelewano yaliyofikiwa kati ya Mwajiri na Mfanyakazi au Mkataba wa Maandishi na Chama chake kwa niaba ya Mwanachama/Wanachama.

(xii) **Akidi:**- Ina maana idadi ya Wajumbe wanaohitajika katika kikao ili kikao kiwe halali na kianze shughuli zake.

(xiii) **Mgogoro:**- Ina maana ya kuwepo kwa hali isiyokuwa ya maelewano kati ya Mwajiri na Mfanyakazi au Wafanyakazi kuhusiana na Ajira kwa ujumla.

(xiv) **Bendera ya Chama:**- Ina maana ya alama ya Chama yenye rangi ya Maziwa, bluu, nyeusi na Nembo ya Chama.

(xv) **Mgomo:**- Ina maana ya kitendo chochote kinachotendwa na Wafanyakazi ambacho kitasababisha uzorotaji Kazi au Kusimama kwa shughuli zinazoendeshwa na Mwajiri kutokana na kutotendwa na Wafanyakazi, na hii ni kutoelewana kati ya Mwajiri na Wafanyakazi kuhusu hali ya masharti ya Kazi.

(xvi) **Mgomo wa kuketi:**- Ina maana ya kuweka Zana chini za Kazi, Wafanyakazi kwenda kazini lakini hawafanyi kazi yoyote bali kuketi kitako tu.

(xvii) **Mgomo wa Wafanyakazi:**-Ina maana ya Wafanyakazi kukataa kufanya Kazi mpaka hapo madai yao yatakapokubaliwa.

(xviii) **Mkataba wa Hali Bora:**- Ina maana makubaliano yaliyofikiwa kati ya Chama na Wafanyakazi na Mwajiri au Chama cha Waajiri kuhusu haki na Mazingira bora ya Kazi na Maslahi kwa Wafanyakazi.

(xix) **Shirikisho:**- Ina maana ya Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania na ambamo Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na afya kimejishirikisha.

(xx) **Mwenyekiti:**- Ina maana Kiongozi Mkuu wa Chama katika Nafasi husika kwa mujibu wa Katiba hii. Ambae atachaguliwa na Mkutano Mkuu miongoni mwa Wanachama wa Chama hiki kwa mujibu wa Katiba.

(xxi) **Naibu Katibu Mkuu:**- Ina maana Mtendaji Mkuu Msaidizi wa Chama.

(xxii) **Sera:**- Ina maana Dira ya Chama inayotoa mwelekeo na mwongozo wa shughuli zote za Chama.

(xxiii) **Mkoa wa (TUGHE):**- Ina maana Mkoa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania. Kama itakavyoamriwa mara kwa mara na Baraza Kuu la Taifa.

(xxiv) **Mkoa:**- Ina maana Mkoa wa Kiserikali na mkoa ulioanzishwa kichama.

(xxv) **Mwajiri:**- Ina maana Mtu binafsi, Kampuni, Shirika, Serikali, Wakala, Taasisi, ambaye ameingia Mkataba wa makubaliano ya maandishi na Mtu fulani kwa madhumuni ya kumtendea Kazi kwa kutoa Fedha au malipo ya Ujira au Mshahara.

(xxvi) **Mweka Hazina:**- Ina maana Mtunza Hazina wa Chama katika Ngazi husika.

(xxvii) **Taifa:**- Ina maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(xxviii) **Kijana:**- Ina maana ni Mwanachama kamili mwenye Umri wa Miaka 18 – 35.

(xxx) **Ulemavu:**- Ina maana ni kukosa au kushindwa kuwa na uwezo wa kufanya Kazi sawa na watu wengine kwa sababu ya Maumbile.

(xxxi) **Wilaya:**- Ina maana Wilaya ya Kiserikali.

(xxxii) **Wilaya ya (TUGHE):**- Ina maana Wilaya ya Chama ni kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu la Taifa kwenye vikao maalumu.

(xxxiii) **Tawi la Chama:**- Ina maana Ngazi ya mwanzo ya Uongozi/Uwakilishi wa Chama.

(xxxiv) **Matawi ya Mseto:**- Ina maana Mahali pa Kazi ambapo Wafanyakazi wake hawajatimia Idadi kwa mujibu wa Muundo wa Tawi, hivyo kuunganishwa pamoja.

(xxxv) **(TUGHE) Taifa:-** Ina maana Makao Makuu ya Chama.

(xxxv) **KUBK:**- Ina maana ni chombo cha utekelezaji na maamuzi kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(xxxvi) **Baraza Kuu:-** Ina maana ni chombo cha maamuzi kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(xxxvii) **Mkutano Mkuu:-** Ina maana ya chombo chenye mamlaka ya juu kabisa katika Uongozi wa Chama.

(xxxviii) **Kamati ya Wanawake:-** Ina maana ya chombo cha Wanawake kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(xxxix) **Serikali:**- Kwa maana ya TUGHE, ina maana ya Serikali Kuu na Wanachama waliogatuliwa kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

SURA YA KWANZA

S. 1 MISINGI YA CHAMA

1:0 Jina la Chama litakuwa “Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania” (TUGHE) au “Tanzania Union of Government and Health Employees” (TUGHE)

1:1 Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania, au Tanzania Union of Government and Health Employees (TUGHE), Barabara ya Jakaya Kikwete, (PLOT No. 5 Block G) Mkoa wa Dodoma. Anuani ya Posta, S.L.P. 2364 **DODOMA.**

1:2 Ofisi ya Makao Makuu ya TUGHE yatakuwa Dodoma, Mkoani Dodoma au mahali popote Tanzania Bara kama itakavyoamriwa na Baraza Kuu la TUGHE.

1:3 Bendera na Nembo ya Chama vimefafanuliwa zaidi katika Kanuni za Chama.

1.4 Chama hiki kitakuwa huru kujishirikisha na SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania na wakati wote kitakapojishirikisha kitajitahidi kuheshimu na kueneza maadili na Sera za SHIRIKISHO hili, ili kuimarisha nguvu ya Umoja wa Wafanyakazi Nchini.

1:5 Chama hiki kinaweza kuwa na uhusiano na Vyama vingine vya Sekta ya Serikali na Afya, Mahakama, Bunge, Wakala wa Serikali, Mamlaka za kukusanya kodi za Serikali na Mamlaka nyingine katika Nchi mbalimbali vyenye malengo sawa na TUGHE, na kina-weza kujiunga na Muungano wa Wafanyakazi wa Kimataifa kila itakapohitajika kufanya hivyo kwa maslahi ya Wanachama.

1:6 Chama kinaamini kuwa:-

(a) Wafanyakazi wote Duniani ni sawa.

(b) Kila Mfanyakazi anastahili malipo ya haki kufuatana na Mkataba wa ajira yake na kuheshimiwa kama Binadamu.

(c) Mshikamano wa Wafanyakazi wote Duniani ndiyo njia pekee itakayokuza ushirikiano wa karibu kati ya Wafanyakazi na Vyama vyao katika Nchi zote.

(d) Nguvu ya Wafanyakazi itatokana na juhudi zao katika kukuza Umoja wao.

(e) Kila Mfanyakazi/Mwanachama atakuwa Huru kujiunga na Chama chochote cha Siasa atakachopendelea.

SURA YA PILI

S. 2 MADHUMUNI YA CHAMA

2:0 Madhumuni makuu ya Chama yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya Wanachama katika maisha yao wakiwa kazini na kufuatilia maslahi yao wakishastaafu.

(b) Kushirikiana na kujadiliana na Waajiri katika kudumisha amani mahali pa kazi.

(c) Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya Mwajiri na Mwanachama, au Mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kila itakapowezekana.

(d) Kushiriki katika kuandaa na kusaidia katika utekelezaji wa Mikataba ya Hali bora za kazi, Tuzo, Kanuni za Nidhamu na kanuni zozote zile ambazo zitatumika Nchini.

(e) Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na Vyama vingine vya Wafanyakazi Nchini pamoja na vile vya Kimataifa kwa madhumuni ya:-

(i) Kupata, kutunza na kutoa taarifa au Elimu katika masuala Muhimu yahusuyo Vyama vya Wafanyakazi.
(ii) Kubadilishana ujuzi au taarifa katika masuala yanayohusiana na Mishahara na hali za Wafanyakazi, na taratibu za Kimataifa zinazohusiana na masuala hayo.

(f) Kuwasiliana na Serikali kuhusu haja ya kutunga Sheria sahihi za kazi na kuandaa Sera nzuri ya jamii.

(g) Kulinda maslahi ya Wanachama kwa kuishinikiza Serikali na Waajiri wengine kuepukana na uandaaji wa Sera ambazo ni hatari kwa Wafanyakazi.

(h) Kutetea na kulinda matakwa na stahiki za Wanachama.

(i) Kusuluhisha na kutatua malalamiko au migogoro ya kikazi kati ya Waajiri na Wanachama au baina ya Wanachama wenyewe kwa wenyewe kwa majadiliano.

(j) Kuhakikisha kwamba Waajiri na Wanachama wanazingatia na kutekeleza vyema matakwa ya Sheria na kanuni za Nchi pamoja na Mikataba iliyopo kati ya Waajiri hao na Chama chao.

(k) Kuwaelimisha Wanachama juu ya masuala yote yanayohusiana na ajira zao, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kisheria pale inapohitajika.

(l) Kuwaunganisha Wafanyakazi wa Serikali na Afya

(m) Kuwekeza katika Vitega Uchumi vitakavyoboresha Ustawi wa Chama ingawa si Chama cha kibiashara.

(n) Kutengeneza na kutetea Sera itakayolinda hadhi ya Wafanyakazi wenye ulemavu waliopo katika sekta za Chama na kuhakikisha kuwa Afya zao, hali zao, haki zao, vinalindwa na kuzuia Vikwazo vinavyoathiri utendaji Kazi wao na kuwa wanapata huduma zao zinazostahili.

(o) Kuhakikisha kuwa Waajiri wanazingatia na kutekeleza Sheria na Kanuni za Nchi zinazohusu Kazi pamoja na Mikataba iliyopo kati ya Waajiri na Wafanyakazi au Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania ili mradi Sheria hizo zilizingatia haki.

(p) Kuhakikisha kuwa sehemu zote za Kazi walipo Wanachama wetu hawapati bughudha ya Kijinsia na kuweka utaratibu utakaodhibiti wale watakaokiuka.

(q) Kuhakikisha Waajiri wote wahusika wanatambua uwepo wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE).

(r) Kuhakikisha Chama kinawakutanisha mara kwa mara ili kujadili maendeleo na matatizo katika Taaluma zao na kutafuta mbinu za kuyatatua, kufahamiana na kubadilishana mawazo ili kufanya utamaduni wa kujiendeleza na kukifahamu Chama chao.

(s) Kutunga na kusimamia Sera itakayolinda hadi ya Wanachama Wanawake kwa kutambua hali na maumbile yao na kuhakikisha Afya zao zinalindwa bila Ubaguzi wa Ajira, likizo ya Uzazi na huduma nyingine anazostahili Mfanyakazi yeyote.

(t) Kuhakikisha Waajiri wanaimarisha usalama wa Wafanyakazi sehemu za kazi

SURA YA TATU

S. 3 UANACHAMA

3.0Wanachama wa TUGHE watatoka katika Sekta zifuatazo: -

i. Sekta ya Serikali Kuu na Afya;
ii. Wizara za Serikali;
iii. Taasisi zilizopo chini ya Wizara.
iv. Wakala za Serikali;
v. Mamlaka za Serikali;
vi. Mahakama;
vii. Bunge;
viii. Mamlaka za kukusanya kodi za Serikali;
ix. Tume na Bodi nchini zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria kwa lengo la kutekeleza majukumu ya Kiserikali;
x. Mamlaka za Maji Mijini na Mabonde ya Maji;
xi. Watumishi wa Sekta ya Afya katika;
    a) Taasisi za Umma;
    b) Serikali za Mitaa;
    c) Taasisi za Dini; na
    d) Taasisi binafsi;
xii. Watumishi wa kada mbalimbali waliogatuliwa kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa na sehemu mbalimbali;
xiii. Watumishi waajiriwa ndani ya Chama cha TUGHE;
xiv. Watumishi wa Maduka yanayotoa huduma za dawa;

3:1 Wanachama wa Chama hiki watakuwa:-

(a) Ni wale ambao walikuwa Wanachama wa Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi (OTTU) na ambao wamerithiwa na Chama hiki kutoka Sekta za hapo juu (3.0) hawa watahesabiwa kama Wanachama waanzilishi.

(b) Ni wale wanaotokana na kifungu 3.0 (i-xiv) na wanachangia asilimia mbili (2%) kwa mujibu wa Katiba kifungu 3.3

(c) Ni Wanachama Waajiriwa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania

(d) Wanachama wa heshima ni Watu Mashuhuri ambao wametoa Mchango maalumu katika malezi na maendeleo ya Chama.

    (i) Uanachama wa heshima utatolewa na Baraza Kuu na unaweza kutunukiwa kwa Wanachama/ Waasisi walio-jitolea wakati wa enzi zao katika kukiendeleza Chama.

    (ii) Wanachama wa heshima hawataruhusiwa kupiga kura katika Mkutano wowote wa Chama.

(e) Ni Wanachuo wenye sifa za taaluma zinazohusiana na Chama chetu walioko ndani na nje ya Nchi yetu.

3:2 Daftari la Wanachama litafuata utaratibu ufuatao:-.

(a) Katibu wa Ngazi husika ataandaa Daftari la Kudumu la kuonyesha majina kamili ya Wanachama walioko katika eneo lake.

(b) Orodha ya Wanachama katika kila Ngazi itaandaliwa kwa kuonesha michango ya Mwanachama kila mwezi kwa mwaka mzima.

(c) Daftari hilo litakuwa wazi kukaguliwa na mtu yeyote kwa kibali cha Katibu wa Ngazi husika kwa kuandika barua yenye kueleza sababu ya kutaka kukagua.

3:3 Mwanachama atalipa asilimia mbili (2%) ya mshahara wake wa kila mwezi kama Ada ya Chama. Kiwango hiki kinaweza kubadilishwa wakati wowote kwa maamuzi ya Mkutano Mkuu.

3:4 Kwa kuwa Wafanyakazi wote wa Serikali na Afya, Mahakama ya Tanzania, Bunge la Tanzania, Wakala wa Serikali na Mamlaka zote za Serikali Nchini wanafaidika na huduma za Majadiliano kati ya Mwajiri na Chama, watawajibika kuchangia Fedha kutoka kwenye Mishahara yao 2% kwa Chama. Wafanyakazi ambao si Wanachama wanaofaidika na huduma za Majadiliano kati ya Chama na Mwajiri watatakiwa kuchangia Fedha kutoka kwenye Mishahara yao asilimia mbili (2%) na kupeleka Fedha hiyo katika Akaunti ya Chama.

3:5 Kila watakapotakiwa Wafanyakazi/Wanachama kuwajibika kutoa michango maalum itakayoamriwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa ya Chama (KUBK) katika masuala mengine yanayohusiana na migomo au masuala mengine ya maslahi ya Chama au Wanachama, watafanya hivyo.

3:6 (i) Kila Mwanachama atapewa Kadi iliyochapishwa ambayo ndani yake itajazwa jina na anwani yake, kazi yake, nambari yake, tarehe ya kujiunga na Chama, Sehemu ya Chama na maelezo mengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Kamati au taratibu za Chama.

(ii) Baada ya kukubaliwa kujiunga na Chama maelezo yote ya Mwanachama huyo yaliyomo katika Kadi ya Uanachama yataingizwa katika Daftari la Kumbukumbu za Chama kwa Kumbukumbu za michango ya Mwanachama na Kumbukumbu hizo zitatakiwa kuwa sahihi kila wakati Tawini, Mkoani na Makao Makuu.

3:7 Mwanachama yeyote mbali na Mwanachama wa heshima, atakuwa na haki zifuatazo:-

(a) Kuwakilishwa na Chama dhidi ya Mwajiri wake pamoja na haki ya yeye mwenyewe kujitetea dhidi ya Mwajiri huyo kwa mashitaka yoyote dhidi yake.

(b) Kujitetea mbele ya vyombo mbalimbali vya Chama na haki ya kuomba rufaa katika vyombo vya juu vya Chama pale ambapo itabidi kama hataridhika na uamuzi uliotolewa.

(c) Kushiriki katika kuchagua na kuchaguliwa katika Uongozi wa Chama kwa mujibu wa Katiba hii.

(d) Kushiriki katika shughuli zozote za Chama na Mikutano kwa mujibu wa Katiba hii.

(e) Kufafanuliwa juu ya hesabu na mali za Chama.

(f) Makao Makuu/Mikoa ihakikishe kwamba Matawi yanapewa na Waajiri asilimia ishirini (20%) ya makusanyo ya ada kwa matumizi ya Matawi, ambayo pia ni haki ya Wanachama Mahali pa Kazi.

(g) Kukata rufaa ya kwenda katika kikao cha juu cha Chama, endapo Mwanachama hakuridhika na uamuzi uliotolewa dhidi yake. Kwa matatizo ya Kichama isipokuwa kwa

Ngazi ya Mkoa itaishia Kamati ya Utendaji, Viongozi wengine wasiochaguliwa na Mkutano Mkuu itaishia Ngazi ya Baraza Kuu.

3:8 Kila Mwanachama atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kulipa Ada ya kila mwezi kwa wakati unaotakiwa na michango maalum kadri ya itakavyoamriwa na vikao halali vya Chama.

(b) Kuunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya Chama.

(c) Kuzingatia Katiba na taratibu za Chama kwa kuheshimu maamuzi yaliyotokana na Katiba au taratibu hiyo.

(d) Kuhudhuria vikao vya Chama vinavyohusika

(e) Kujua haki zake

(f) Kukilinda, Kukitangaza na Kukitetea Chama wakati wote na kwa nguvu zote.

(g) Kutekeleza maamuzi ya Chama.

(h) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama.

3:9 Mwanachama ataorodheshwa katika daftari Kuu la Chama kwa Jina lake kamili na taarifa nyingine zinazomhusu.

3:10 Mwanachama atakoma kuwa Mwanachama iwapo:-

(a) Hatatoa Ada yake kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo bila sababu maalum zinazohusiana na Ajira yake

(b) Akikoma kuwa Mfanyakazi wa Kuajiriwa kutokana na sababu zozote zile.

(c) Hatakuwa Mfanyakazi wa Kuajiriwa Kazi au Kufukuzwa Kazi na Chama kuridhika kuwa kufukuzwa kwake ni halali.

(d) Atajiuzulu

(e) Atafukuzwa Uanachama

(f) Atafariki Dunia

(g) Atastaafu

(h) Mwanachama atakoma uanachama iwapo atastaafu utumishi kwa mujibu wa umri.

(i) Mwanachama akikoma Uanachama hatarudishiwa Ada zake zozote alizotoa.

3:11 Mwanachama ni lazima awe na Maadili ya Kazi yake kama yalivyo katika Sheria za Nchi ili mradi zinazingatia haki.

3:12 (a) Mwanachama atafukuzwa iwapo atathibitika kwamba amekosea Uzalendo na Utii kwa Chama. Kwa Mfano kuhusiana na masuala ya kukisaliti Chama, Uchochezi wa Migogoro ya Kikazi.

(b) Halmashauri ya Tawi itatoa taarifa ya ushauri wake kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa ya Chama ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya kumfukuza Mwanachama.

(c) Baada ya kujadili, Kamati ya Utendaji ya mkoa itapeleka taarifa ya mapendekezo yake kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa (KUBK).

(d) Kamati ya Utendaji ya Taifa (KUBK) itatoa uamuzi na kuupeleka kwa Mwanachama kupitia kamati ya Utendaji Mkoa na Halmashauri ya Tawi itapewa nakala.

(e) Mwanachama aliyefukuzwa Uanachama na Kamati ya Utendaji ya Taifa atakuwa na haki kuomba rufaa dhidi ya uamuzi huo kwenye Baraza Kuu la Taifa.

(f) Endapo ni Kiongozi na amejihusisha katika kukisaliti, kukihujumu, kuvunja Katiba au kutenda kosa lenye kukiuka maadili au kumwondolea sifa za kuwa Kiongozi atasimamishwa Uongozi na mapendekezo yatapelekwa kwa Mamlaka iliyomchagua kwa maamuzi.

3:13 Mwanachama anayehama sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine katika Chama hiki atatoa taarifa katika Tawi anapokkwenda au Tawi la karibu na kuendelea kuwa Mwanachama wa Chama hiki.

SURA YA NNE

S. 4 OFISI ZA CHAMA

4:0 Chama kitakuwa na Ofisi zifuatazo katika kutoa huduma zake kwa Wanachama:-

Tawi, Mkoa na Taifa.

4:1 (a) Tawi litakuwa ndiyo ngazi ya mwanzo ya Uongozi/Uwakilishi wa Chama na litakuwa kila sehemu ya kazi yenye Wanachama sawa na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura 366 marejeo ya 2019 Kif. 62.

(b) Mahali ambapo Wafanyakazi Wanachama hawakidhi mahitaji ya Sheria ya Idadi ya Wanachama, watajiunga na mahali pengine pa Kazi palipo karibu ili kuunda Tawi la Mseto.

(c) Matawi haya yataundwa kwa uamuzi wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(d) Halmashauri ya Tawi litakaloundwa kwa mujibu wa Kif. 4.1 (b) hapo juu itachagua mwakilishi wa kila mahali pa kazi ambapo Wanachama wake wamejiunga na Tawi hilo.

4.2 (a) Mkoa wa TUGHE ni Mkoa wa Kiserikali na Makao Makuu yake yatakuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Kiserikali Tanzania Bara kila Mkoa utasimamia kazi zote za Chama katika eneo la Mkoa huo.

(b) Mkoa wa TUGHE utaanzishwa kwa Mamlaka ya Baraza Kuu la Taifa.

(c) Mkutano wa Baraza Kuu unaweza kuamua kuanzisha Mkoa ndani ya Mkoa wa Kiserikali kutegemeana na mahitaji ya wakati huo.

4.3 Makao Makuu ya TUGHE yatakuwa Dodoma au mahali pengine Tanzania Bara kama itakavyokuwa ikiamriwa na Baraza Kuu, ambapo patakuwa Ngazi ya juu kabisa kitaifa katika Uongozi wa Chama na yatasimamia shughuli za Chama Nchini.

SURA YA TANO

S. 5 VIONGOZI/MAAFISA WAKUU WA CHAMA NA KAZI ZAO

TAWI

5:0 Mwenyekiti wa Tawi atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli za Chama Tawini na msemaji Mkuu wa Sera za Chama katika ngazi hii.

(b) Ataongoza mikutano yote ya Tawi na kuweka saini kwenye Mihtasari ya mikutano.

(c) Licha ya kura yake ya kawaida katika maamuzi atakuwa na kura ya turufu.

(d) Kama Mwenyekiti hayupo, Mjumbe yeyote wa kikao hicho anaweza kuteuliwa kukiongoza kikao hicho.

5:1 Katibu wa Tawi atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli za Chama Tawini na msemaji wa shughuli za kila siku za Chama katika Tawi.

(b) Ataitisha mikutano yote ya Tawi kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Tawi, kwa mujibu wa Katiba hii.

(c) Kuandika na kutunza Kumbukumbu za Mikutano yote ya Tawi.

(d) Kutunza vitabu vya hesabu za Fedha na mali za Tawi na Kuendeleza vipindi vya mwaka wa Fedha.

(e) Kuwasilisha kwa Katibu wa Mkoa Fedha zote alizopokea kwa niaba ya Tawi kila mwezi baada ya kuondoa fedha ambazo ameruhusiwa kubakiza kwa matumizi ya Tawi.

(f) Kuandaa taarifa ya kila mwezi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Tawi itakayoonesha kwa usahihi Mapato na Matumizi ya Tawi na kumpa taarifa Katibu wa Mkoa kuhusiana na michango.

(g) Kuwasilisha kwa Katibu wa Mkoa taarifa ya Wanachama wote katika Tawi pamoja na tarehe walipojiunga na Chama, namba za Kadi zao na maslahi ya malipo kwa Wanachama husika.

(h) Kufanya mawasiliano yote yanayo husika katika Tawi na kuwasomea/kuwaeleza Wanachama.

(i) Kusimamia masuala ya Usajili wa Wanachama na kuhakikisha kuwa wanadumu katika Chama.

(j) Kusimamia na kuimarisha demokrasia Mahala pa Kazi.

(k) Kuwawakilisha Wanachama katika masuala ya Afya, Usalama Kazini na Ustawi wa Jamii.

(l) Kuwawakilisha Wanachama katika Migogoro ya kikazi na masuala ya Kinidhamu pamoja na kusimamia utatuzi wa Migogoro ya Wanachama Sehemu za kazi.

(m) Kukiwakilisha Chama katika Uchunguzi wa utekelezaji wa Sheria za Kazi unaoendeshwa na Wakaguzi wa Kazi.

(n) Kupokea maagizo au taarifa kutoka Ngazi ya Mkoa, kusimamia utekelezaji wake na kutoa muitikio kwa Uongozi wa Mkoa.

(o) Kuwajibika kwa ngazi zilizopo juu yake.

(p) Kusajili Wanachama.

(q) Kutunza mali za Chama.

(r) Kuratibu Mkutano Maalumu wa Wilaya akishirikiana na Mratibu.

(s) Kama atakoma kuwa Katibu kwa sababu yoyote ile, isipokuwa Kifo, atawasilisha kwa Halmashauri ya Tawi fedha zote, vitabu na mali za Chama au mauzo ya mali hizo.

5.1A Mratibu wa Wilaya atafanya kazi zifuatazo:

(a) Atamsaidia Katibu wa Mkoa kuratibu shughuli zote za Chama kwenye Wilaya.

(b) Atakuwa kiungo kati ya Tawi na Mkoa

(c) Atamsaidia Katibu wa Mkoa kuratibu Mikutano ya Chama kwenye Wilaya.

(d) Atatekeleza Majukumu mengine yanayohusu Chama kama atakavyoelekezwa na Katibu wa Mkoa na atatoa taarifa za hali ya Chama Wilayani kwake kila baada ya miezi 6 kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

MKOA

5.2 Mwenyekiti wa Mkoa atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) Ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli za Chama Mkoani na msemaji Mkuu wa Sera za Chama katika ngazi hii.

(b) Kuongoza Mikutano yote ya Chama katika ngazi ya Mkoa na Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao Kitaifa.

(c) Licha ya kura yake ya kawaida katika maamuzi atakuwa na kura ya turufu.

(d) Kama Mwenyekiti hayupo, Mjumbe yeyote miongoni mwa Wajumbe wa Kamati anaweza kuteuliwa kukiongoza kikao.

(e) Kutoa msimamo wa Sera za Chama kama zitakavyoamriwa na vikao vya Chama Kitaifa.

(f) Kuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Chama katika Mkoa na Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya Taifa.

(g) Kuwa mwangalizi wa karibu kwa Matawi yote yaliyoko Mkoani mwake.

5:3 Katibu wa Mkoa atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Ndiye Mtendaji na Msemaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Mkoa

(b) Kuitisha Mikutano yote ya Chama Mkoani kwa mujibu wa Katiba baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Mkoa.

(c) Kutunza vitabu vyote vya Fedha na Hati kwa mujibu wa Kanuni za Fedha na Katiba ya Chama.

(d) Kuandika na kutunza Kumbukumbu za mikutano yote ya Mkoa.

(e) Kupeleka Fedha zote Benki, alizozikusanya kutoka katika Matawi yote Mkoani mwake.

(f) Kuwasilisha kila nusu mwaka taarifa ya fedha mbele ya Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(g) Kupeleka ajenda kwa kila Mjumbe wa mkutano wa Mkoa angalau siku 14 kabla ya tarehe ya Mkutano wa Kamati ya Utendaji na siku 28 kabla ya Mkutano Mkuu.

(h) Kuishauri Kamati ya Utendaji ya Mkoa katika kusimamia Uchaguzi Mkoani.

(i) Kuwasilisha taarifa ya kazi za Chama na Mapato/Matumizi ya Mkoa kwa Katibu Mkuu wa Chama kwa mujibu wa taratibu za Chama.

(j) Kusimamia shughuli zote za Chama ikiwa ni pamoja na fedha na mali za Chama katika Mkoa wake.

(k) Kuwa Katibu wa vikao vyote vya Mikutano ya Mkoa.

(l) Kuweka Kumbukumbu za shughuli za Chama katika Mkoa.

(m) Kufuatilia Makato ya Fedha za Wanachama kutoka kwa Waajiri katika Mkoa.

(n) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za shughuli za Chama katika kipindi husika.

(o) Kuhamasisha na kuingiza Wanachama wapya.

(p) Kuratibu kikao maalumu cha Wilaya akishirikiana na Mratibu wa Wilaya.

TAIFA

5:4 Mwenyekiti wa Taifa atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli za Chama kwa mujibu wa Katiba na Msemaji wa Sera za Chama Kitaifa.

(b) Kuhakikisha Katiba, Kanuni na taratibu za Chama zinafuatwa na wale wote wanaohusika.

(c) Kuongoza Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu, na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(d) Kuweka saini kwenye Kumbu-kumbu na Mihtasari ya mikutano yote atakayoiongoza.

(e) Licha ya kura yake ya kawaida katika maamuzi atakuwa na kura ya turufu.

(f) Kama Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataongoza kikao.

(g) Kutoa msimamo wa Sera za Chama kama ilivyoamriwa na vikao vya Chama vya Taifa.

5:5 Kutakuwepo na Makamu wa Mwenyekiti atakayechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama ambaye atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuwa Msaidizi Mkuu wa Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

(b) Makamu Kiongozi wa Chama.

(c) Kuongoza vikao vya Taifa kama Mwenyekiti hayupo.

(d) Kuwa Kaimu wa Mwenyekiti kama Mwenyekiti hayupo.

5:6 Katibu Mkuu atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Ndiye Mtendaji Mkuu na Msemaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Chama atakayewajibika katika utekelezaji wa maamuzi yaliyokwishapitishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(b) Kuitisha vikao kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Taifa na kuhudhuria kama Katibu, Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu, Kamati ya Utendaji ya Taifa na mikutano mingine ambayo Kamati ya Utendaji ya Taifa itaamua.

(c) Kutunza Kumbukumbu za mikutano, nyaraka zote muhimu za Chama na kutekeleza Sera za Chama.

(d) Kutayarisha na kuwasilisha Taarifa ya Mapato na Matumizi ya fedha za Chama mbele ya Kamati ya Utendaji ya Taifa, siyo chini ya nusu mwaka na kila mwisho wa mwaka wa Fedha, na kuwasaidia wakaguzi wa hesabu za Chama atakapotakiwa kufanya hivyo.

(e) Kuwajibika kwa Chama kuhusu fedha zote zinazopitia mikononi mwake.

(f) Kutunza Kitabu cha Fedha na vitabu vingine vya Hesabu za Fedha Makao Makuu, kutunza Fedha za matumizi ya kila siku, kufanya malipo kwa niaba ya Chama na kutunza nakala zote za Stakabadhi za Mapato na Matumizi.

(g) Kutoa Stakabadhi kwa Fedha yote iliyopokelewa na Chama.

(h) Kutayarisha Hati za malipo na Hundi zote ambazo zitasainiwa na angalau Mdhamini mmoja na katibu Mkuu au Msaidizi wake. Hati zote hizi zitapokelewa na kupitishwa na Kamati ya Utendaji ya Chama.

(i) Kutoa taarifa na kupeleka kwa kila Mjumbe Agenda za mikutano angalau siku 14 kabla ya Mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Mkoa, siku 21 kabla ya Baraza Kuu na siku 30, kabla ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa.

(j) Kusimamia shughuli za uendeshaji za kila siku za Chama.

(k) Kuhusika na kutoa Kadi kwa Wanachama na Vitambulisho kwa Wafanyakazi wa Chama.

(l) Kufuatilia Makato ya Ada za Wanachama kutoka kwa Makatibu wa Mikoa na Waajiri.

(m) Mkuu wa Watumishi wote wa Chama.

(n) Mdhibiti Mkuu na Mhifadhi wa Fedha na Mali za Chama katika Ngazi zote.

5:7 Kutakuwa na Manaibu Katibu Mkuu wawili katika Sekta za Serikali na Afya watakaomsaidia Katibu Mkuu kwa shughuli za siku hadi siku pamoja na utaratibu ufuatao:-

(a) Naibu Katibu Mkuu atakaye-shughulikia Fedha, Utawala, Utumishi na utetezi, na atakuwa Mweka hazina wa Chama.

(b) Naibu Katibu Mkuu atakayeshughulikia Elimu, Oganaizesheni, mahusiano ya Kimataifa, utetezi na jinsia.

(c) Watakuwa Makaimu Katibu, atakapokuwa amependekezwa mmoja wapo kama hatakuwepo Katibu Mkuu.

SURA YA SITA

S. 6 VIKAO VYA CHAMA

6:0 Tawi litakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano wa Wanachama wote

(b) Mkutano wa Wafanyakazi wote

(c) Halmashauri ya Tawi.

MKUTANO WA WANACHAMA WOTE

6:1 (a) Mkutano wa Wanachama wote utajumuisha Wanachama wote katika Sehemu ya Kazi kama ni Tawi la Muungano.

(b) Mkutano huu utafanywa mara mbili kwa mwaka, lakini kikao cha dharura kinaweza kuitishwa wakati wowote.

(c) Ni Wanachama hai tu wanaoruhusiwa kuhudhuria Mkutano wa Wanachama wote.

6:2 Mkutano wa Wanachama wote utakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taarifa za Halmashauri ya Tawi na kuiagiza Halmashauri hiyo kutekeleza maamuzi ya Mkutano huo.

(b) Kupokea na kujadili njia za kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa na Vyombo vya Mkoa, Taifa na Wanachama wenyewe katika Tawi.

(c) Wakati wa Uchaguzi, Mkutano wa Wanachama wote utawachagua viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Halmashauri ya Tawi.

(iv) Mwakilishi mmoja wa Walemavu

(v) Mwakilishi mmoja wa Vijana

(d) Kujadili na kupitisha Bajeti na mipango ya mwaka ya kazi za Chama Sehemu ya Kazi.

(e) Kujadili na kupokea taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Chama kwa kipindi cha miezi sita.

(f) Kubuni njia mbalimbali za kuimarisha Chama na Ustawi wa Wanachama.

(g) Kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zitokazo Ngazi za juu za Chama.

(h) Kumwondoa madarakani kiongozi wa Chama wa Sehemu ya Kazi akipatikana na hatia baada ya kupewa fursa ya kusikilizwa.

MKUTANO WA WAFANYAKAZI WOTE

6:3 (a) Mkutano wa Wafanyakazi wote utajumuisha Wafanyakazi wote katika Sehemu ya Kazi.

(b) Mkutano wa Wafanyakazi wote utafanyika mara moja kwa mwaka lakini mikutano ya dharura inaweza kuitishwa wakati wowote.

6:4 Mkutano wa Wafanyakazi wote utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kujadili utekelezaji wa Mpango wa Kazi kama ulivyowasilishwa na Halmashauri ya Tawi.

(b) Kujadili taarifa ya utekelezaji kazi itakayowasilishwa na Mkutano wa Wanachama wote na Baraza la Wafanyakazi.

HALMASHAURI YA TAWI

6:5 Halmashauri ya Tawi itaundwa na wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Tawi

(b) Katibu wa Tawi

(c) Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi kwa kuzingatia idadi ya Wanachama kama ifuatavyo:-

(i) Wajumbe watatu kama Tawi halina zaidi ya Wanachama hamsini.

(ii) Wajumbe wanane kama Tawi lina Wanachama zaidi ya hamsini lakini hawazidi mia moja.

(iii) Wajumbe kumi na tatu kama Tawi lina Wanachama wanaozidi mia lakini hawazidi mia tano.

(iv) Wajumbe kumi na nane kama Tawi lina Wanachama wanaozidi mia tano lakini chini ya elfu moja.

(v) Wajumbe ishirini na tatu kama Tawi lina Wanachama wanaozidi elfu moja.

(d) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Tawi.

(e) Mwakilishi mmoja wa Walemavu.

(f) Mwakilishi mmoja wa Vijana.

6:6 Halmashauri ya Tawi itakutana mara moja kila mwezi lakini inaweza kufanya vikao vya dharura wakati wowote.

6:7 Halmashauri ya Tawi itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kutetea na kulinda ajira, haki za Wafanyakazi ikiwa ni pamoja kujadili masharti ya Utumishi kwa Wanachama wake na kuhakikisha kuwa Afya na Usalama vinadumishwa Mahali pa Kazi.

(b) Kuwasilisha Mikataba ya Hiari katika Kamati ya Utendaji ya Chama ya Mkoa na kuiarifu kuhusu suala lolote ambalo linaweza kusababisha Mgogoro wa Kikazi.

(c) Kubuni njia za Tija na kuendeleza uzalishaji na Ajira ya uhakika na kuhakikisha kuwa Wanachama wanafaidika kutokana na ziada inayotolewa na ongezeko la Tija.

(d) Kutoa taarifa mara kwa mara kwa Wanachama kuhususshughuli za Tawi kwa ujumla.

(e) Kuingiza Wanachama wapya.

(f) Kuendeleza uhusiano mwema na Matawi mengine.

(g) Kuchagua Katibu wa Elimu wa kuendesha Elimu ya Wafanyakazi.

(h) Katika Matawi makubwa, Halmashauri itachagua wawakilishi wenye kazi maalumu ya kuwasiliana na Wanachama katika Idara au sehemu mbalimbali Mahali pa Kazi.

(i) Kutoa misaada kwa Wanachama

(j) Kupanga na kudhibiti Mapato na Matumizi ya Tawi.

(k) Kuendeleza Kitabu cha Kumbu-kumbu za Wanachama na Wafanyakazi.

(l) Endapo kutatokea mgogoro wa kikazi Mahali pa Kazi, Halmashauri ya Tawi itaitisha Mkutano wa Wanachama wote na kama ni mahali ambapo muafaka na Mwajiri umeshindikana, kura ya maoni ya kuhusu uwezekano wa kuitisha mgogoro itapigwa. Uamuzi wa kutangaza mgogoro utahitaji theluthi mbili ya Wanachama na itawasilishwa mbele ya Mkoa ili itoe kibali, baada ya kushauriana na Makao Makuu ya Chama.

6:8 Kutakuwepo na Kamati ya Wanawake chini ya uongozi wa Halmashauri ya Tawi ambayo itachaguliwa miongoni mwa Wanawake Wanachama waliomo katika Tawi.

6:9 Kamati ya Wanawake ya Tawi itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(1) Mwenyekiti

(2) Katibu

(3) Mweka Hazina

(4) Wajumbe wawili wa Kamati

6:10 Kamati ya Wanawake ya Tawi itakuwa na kazi zifuatazo:-

(1) Kuwaunganisha Wanawake wote kwenye Tawi.

(2) Kuwakilisha maoni na matatizo ya Kijinsia katika Halmashauri ya Tawi.

(3) Kubuni na kutekeleza mipango ya kimaendeleo ya Wafanyakazi Wanawake Tawini.

6:11 Taratibu za Uchaguzi Tawini:-

(a) (i) Ni Wanachama hai tu waliotimiza angalau mwaka mmoja katika Tawi wenye haki ya kuomba Uongozi isipokuwa pale ambapo Tawi ni jipya.

(ii) Bila ya kuathili Kifungu (i) hapo juu, kila Mwanachama Hai Tawini ana haki ya kupiga na kupigiwa kura Tawini kwake.

(b) Wakati wa Uchaguzi au kujaza nafasi wazi, kila Mwanachama anayestahili atajaza fomu ya kuomba nafasi anayoihitaji na kuirejesha katika Ofisi ya Katibu wa Tawi.

(c) Mkutano utamchagua Mjumbe yeyote asiyegombea nafasi yoyote kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo.

(d) Wakati wa Uchaguzi mdogo Tawini, Katibu (au Mwenyekiti kama nafasi ya Katibu ndiyo iko wazi) ataitangaza nafasi hiyo kuwa wazi na kuwaruhusu Wanachama wanaotaka wajaze fomu na kuzirejesha Ofisi ya Tawi angalau siku saba (7) kabla ya Uchaguzi.

(e) Taarifa ya matokeo ya Uchaguzi mara tu baada ya kutangazwa kumbukumbu za matokeo zitahifadhiwa Tawini na nakala kupelekwa Mkoani au Makao Makuu.

MKUTANO MAALUM WA WILAYA

6:12 (a) Kutakuwa na Mkutano maalum wa Wilaya katika Wilaya za Kiserikali.

(b) Wajumbe wa Mkutano maalum wa Wilaya ni hawa wafuatao:-

(i) Wenyeviti wa Matawi ya TUGHE Wilayani.

(ii) Makatibu wa Matawi ya TUGHE Wilayani.

(iii) Mratibu wa Wilaya.

(iv) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Wanawake za Matawi yaliyopo Wilayani

(v) Mwakilishi wa Walemavu.

(vi) Mwakilishi wa Vijana

6:13 Mkutano maalum wa Wilaya utafanya kikao chake kila baada ya miaka miwili na nusu. Bila kuathiri muda uliowekwa, Katibu wa Mkoa anaweza kuitisha Mkutano wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi iwapo nusu au zaidi ya Wajumbe wa Wilaya hiyo, kwa sababu yoyote ile, wamekoma kuwa Viongozi.

6:14 Mkutano Maalum wa Wilaya utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuchagua Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kutokana na orodha yao, miongoni mwao angalau wawili wawe Wanawake.

(b) Kuchagua mwakilishi mmoja wa Walemavu.

(c) Kuchagua mwakilishi mmoja wa Vijana.

(d) Kuchagua Mratibu wa Wilaya

(e) Kujumuisha mambo muhimu ambayo matawi yangependa Mkoa uyashughulikie kwa pamoja, kwa haraka au kwa upendeleo maalum.

(f) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.14 (a-d) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka mitano.

6:15 Kutakuwa na Mkutano wa Wanawake wa Wilaya ya kila eneo la Wilaya ya Kiserikali.

6:16 Mkutano wa Wanawake wa Wilaya utakuwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Wenyeviti wa Kamati za Wanawake waliomo Wilayani.

2. Makatibu wa Kamati za Wanawake waliomo Wilayani.

6:17 Mkutano wa Wanawake wa Wilaya utafanya kazi zifuatazo:-

1. Kuwaunganisha Wanachama Wanawake wote waliomo kwenye Wilaya.

2. Kutoa maoni na kutetea masuala yote Kijinsia kwa ujumla.

3. Kuchagua Wajumbe Wanawake wawili wa kuhudhuria Mkutano wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

4. Bila ya kuathili Kifungu 6.17 (3) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka mitano.

6:18 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itasimamia Mkutano Maalum wa Wilaya ulioratibiwa na Mratibu wa Wilaya.

VIKAO VYA MKOA

6:19 Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya Mkoa:-

(a) Mkutano Mkuu wa Mkoa

(b) Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

MKUTANO MKUU WA MKOA

6:20 (a) Mkutano Mkuu wa Mkoa ndicho chombo kikuu cha Chama katika Mkoa na utafanya kikao chake mara moja kila baada ya miaka mitano, lakini Mkutano wa dharura unaweza kuitishwa wakati wowote kwa kibali cha KUBK.

(b) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Kazi utakaofanyika kila baada ya miaka miwili na nusu tangu kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa kawaida.

6:21 Wafuatao watakuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa:-

(a) Mwenyekiti wa Mkoa

(b) Katibu wa Mkoa

(c) Wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wawili watatoka Sekta ya Serikali, Mahakama, Bunge, Wakala na Mamlaka za Serikali na wawili watatoka Sekta ya Afya

(d) Mjumbe wa Baraza Kuu kutoka Mkoani.

(e) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa.

(f) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Maalum wa Wilaya.

(g) Wajumbe wa Baraza Kuu waliomo katika Mkoa huo.

(h) Waratibu wa Wilaya.

(i) Mwakilishi mmoja wa Walemavu.

(j) Mwakilishi mmoja wa Vijana.

(k) Wajumbe wanne wa Mkutano Mkuu wa Taifa wanaofanya kazi katika Mkoa husika

6:22 Mkutano Mkuu wa Mkoa utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taarifa zilizo-wasilishwa kwake na Kamati ya Utendaji ya Mkoa na kuielekeza Kamati hiyo na kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa kutokana na ajenda hizo na nyingine.

(b) Kujadili na kuratibu njia za kutekeleza Mkoani maazimio yaliyotolewa na vyombo vya juu.

(c) Wakati wa Uchaguzi, Mkutano Mkuu wa Mkoa utawachagua:-

(i) Mwenyekiti wa Mkoa

(ii) Wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wawili watatoka Sekta ya Serikali, Mahakama, Bunge, Wakala na Mamlaka za Serikali na wawili watatoka Sekta ya Afya

(iii) Wajumbe wanne watakaowakilisha Mkoa katika Mkutano Mkuu wa Chama Taifa, kati yao wawili kutoka kila Sekta Mjumbe mmoja Mwanamke na mwingine Mwanamume

(iv) Mjumbe wa Baraza Kuu toka Mkoani.

(v) Mwakilishi mmoja wa Walemavu.

(vi) Mwakilishi mmoja wa Vijana.

(d) Bila kuathiri Kifungu kidogo cha 6.22 (c) (i-vi) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa Uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka mitano.

KAMATI YA UTENDAJI YA MKOA

6:23 Wafuatao watakuwa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa:-

(a) Mwenyekiti wa Mkoa

(b) Katibu wa Mkoa

(c) Wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wawili watatoka Sekta ya Serikali, Mahakama, Bunge, Wakala na Mamlaka za Serikali na wawili watatoka Sekta ya Afya

(d) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa.

(e) Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa, Wajumbe wanne wa Mkutano Mkuu Taifa na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu (KUBK), Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa wanaofanya kazi katika Mkoa husika watakuwa waalikwa katika kikao cha Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(f) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Walemavu ambaye atakuwa Mwenyekiti wa wanachama wenye ulemavu katika ngazi ya Mkoa

(g) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Vijana ambaye atakuwa Mwenyekiti wa wanachama Vijana katika ngazi ya Mkoa.

(h) Waratibu wa Wilaya katika mkoa husika

6:24 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itakutana angalau mara moja kila baada ya miezi sita.

6:25 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kutekeleza maazimio, maagizo na maelekezo ya vikao vya ngazi za juu yake.

(b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Chama katika Mkoa.

(c) Kupokea na kushughulikia taarifa ya Katibu wa Mkoa juu ya maendeleo ya Chama Matawini.

(d) Kuwasilisha mbele ya Mkutano Mkuu wa Mkoa Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Chama kwa kipindi cha Miaka miwili na nusu.

(e) Kutangaza mapema nafasi wazi zinazochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa ili ziweze kujazwa katika Mkutano wa Mkoa unaofuata.

(f) Kuandaa Ajenda na tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(g) Kusimamia vyombo, Mali na Miradi ya Kiuchumi ya Chama katika Mkoa.

(h) Kuwasimamisha Uongozi viongozi waliochaguliwa ngazi ya Mkoa wakipatikana na hatia baada ya kuwapa fursa ya kusikilizwa.

(i) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Chama kwa kipindi cha miezi Sita.

6:26 Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Kamati ya Wanawake Mkoa katika kila Mkoa wa Serikali chini ya Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

6:27 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa watakuwa ni Wajumbe wawili waliochaguliwa na Kamati ya Wanawake ya kila Wilaya .

6:28 Kazi za Mkutano wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa ni:-

(1) Kuwaunganisha Wanawake wote waliomo kwenye Mkoa.

(2) Kutoa maoni ya kutetea masuala ya Kijinsia na maendeleo yao.

(3) Wakati wa Uchaguzi watawa-chagua:-

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

(ii) Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa.

(iii) Mweka hazina wa Kamati ya Wanawake ya Mkoa.

(iv) Wajumbe wawili wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

(4) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.28 (3) (i-iv) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka kumi.

VIKAO VYA TAIFA

6:29 Kutakuwa na vikao vifuatavyo katika ngazi ya Taifa:-

(a) Mkutano Mkuu wa Taifa

(b) Baraza Kuu

(c) Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu.

MKUTANO MKUU WA TAIFA

6:30 Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa, ambao ndiyo kikao chenye mamlaka ya mwisho ya maamuzi katika Chama.

6:31 Wafuatao watakuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa

(b) Makamu Mwenyekiti

(c) Katibu Mkuu

(d) Manaibu Katibu Mkuu.

(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(f) Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(g) Wajumbe wote wa KUBK

(h) Wenyeviti wa Mikoa

(i) Makatibu wa Mikoa

(j) Wajumbe wote wa Baraza Kuu

(k) Wajumbe wanne waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Mkoa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Taifa

(l) Wenyeviti wa Mikoa wa Kamati za Wanawake

(m) Makatibu wa Mikoa wa Kamati za Wanawake.

(n) Mwakilishi wa Walemavu aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu Taifa

(o) Mwakilishi wa Vijana aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu Taifa

6:32 (a) Mkutano Mkuu wa Taifa utafanya kikao chake cha kawaida mara moja katika kipindi cha miaka mitano, lakini unaweza kukutana kwa dharura wakati wowote ukiitishwa na Katibu Mkuu wa Chama au ukiombwa na theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Baraza Kuu.

(b) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Kazi utakaofanyika kila baada ya miaka miwili na nusu tangu kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa kawaida.

6:33 Taarifa ya kufanya Mkutano Mkuu wa Taifa ni lazima itolewe si chini ya siku thelathini kabla ya tarehe ya kukutana lakini inaweza kutolewa taarifa ya muda mfupi zaidi kwa Mkutano wake wa dharura.

6:34 Mkutano Mkuu wa Taifa utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kufanya mabadiliko ya Katiba na kuamua ni lini utekelezaji wake utaanza kutumika au kusitishwa kwa uamuzi wa theluthi mbili ya Wajumbe wenye haki ya kupiga kura.

(b) Kukubali, kubadili au kukataa uamuzi wowote uliotolewa na kikao chochote cha chini yake.

(c) Kujadili Ajenda zinazowasilishwa kwake na Baraza Kuu, kuzitolea uamuzi na kuelekeza utekelezaji wa maamuzi yatokanayo na Ajenda hizo pamoja na mambo mbalimbali yatakayojitokeza katika Mkutano.

(d) Kupokea na kujadili taarifa ya Kazi za Chama ya miaka Mitano.

(e) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Mkutano Mkuu wa Taifa utawachagua Viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Taifa

(ii) Makamu Mwenyekiti

(iii) Katibu Mkuu

(iv) Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya TUCTA

(v) Wajumbe wa Baraza Kuu TUCTA

(vi) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa TUCTA.

(vii) Mwakilishi mmoja wa Walemavu

(viii) Mwakilishi mmoja wa Vijana

f) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.34 (e) (i-vii) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka kumi isipokuwa Wajumbe wa Baraza Kuu na Mkutano Mkuu TUCTA.

6:35 Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Kamati ya Wanawake Taifa ambao utakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa

(ii) Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa

(iii) Wajumbe Wanawake wote wanaohudhuria Mkutano Mkuu wa Taifa

6:36 Mkutano Mkuu wa Kamati ya Wanawake Taifa utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuwaunganisha Wanawake kujiunga kugombea katika Uchaguzi kwa ngazi zote.

(b) Kuweka na kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa Masuala yanayohusiana na tofauti za Kijinsia na maendeleo yao.

(c) Wakati wa Uchaguzi utawachagua wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(ii) Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(d) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.36 (c) (i-ii) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka kumi.

BARAZA KUU

6:37 Baraza Kuu la Taifa litakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa.

(b) Makamu wa Mwenyekiti

(c) Katibu Mkuu

(d) Manaibu Katibu Mkuu

(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(f) Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(g) Wajumbe wa KUBk

(h) Wenyeviti wa Mikoa

(i) Makatibu wa Mikoa

(j) Mjumbe mmoja wa Baraza Kuu toka kila Mkoa.

(k) Wenyeviti wa Mikoa wa Kamati za Wanawake.

(l) Makatibu wa Mikoa wa Kamati za Wanawake.

(m) Mwakilishi mmoja wa Walemavu

(n) Mwakilishi mmoja wa Vijana.

6:38 Baraza Kuu litakutana mara moja kwa mwaka lakini Kamati ya Utendaji inaweza kuitisha kikao maalum cha Baraza Kuu kama theluthi moja ya Wajumbe wa Baraza Kuu wametaka hivyo kwa maandishi.

6:39 Baraza Kuu la Taifa litafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka yatakayowasilishwa kwake na Kamati ya Utendaji.

(b) Kupitia na kuhakiki taarifa ya hesabu za Fedha za Chama zilizokaguliwa.

(c) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

(d) Kutathimini utekelezaji wa shughuli za Chama na kutoa mwelekeo wa maendeleo ya Chama.

(e) Kuamua juu ya uanzishaji wa Mkoa mpya.

(n) Kutunga Kanuni mbalimb ali za Chama kulingana na mahitaji na kuzirekebisha pindi inapobidi.

(o) Kuchukua hatua za Kinidhamu dhidi ya Viongozi wa Kitaifa wanaochaguliwa na mkutano Mkuu, hii ikiwa ni pamoja na kuonya na kuwa simamisha uongozi wakati ukisubiriwa uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(p) Kuteua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Muda inapotokea hawapo kwa mujibu wa Katiba.

(q) Wakati wa Uchaguzi, Baraza Kuu litafanya yafuatayo:-

(i) Kuwachagua Manaibu Katibu Mkuu wawili, mmoja kutoka kila sekta za Chama

(ii) KUchagua Wajumbe kumi wa Kamati ya Utendaji, watano kutoka kila sekta za Chama na kila sekta Wajumbe wasiopungua wawili wawe Wanawake.

(iii) Kuwathibitisha Wadhamini waliochaguliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(r) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.39 (q) (i-ii) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka kumi.

6:40 Kutakuwa na Kamati ya Wanawake ya Baraza Kuu la Taifa ambayo Wajumbe wake watakuwa ni Wajumbe Wanawake wote wa Baraza Kuu la Taifa.

6:41 Kazi kubwa ya Kamati ya Wanawake ya Baraza Kuu la Taifa ni kuweka na kupendekeza masuala yote ya jinsia na maendeleo ya Wanawake kwenye Mkutano Mkuu wa Kamati ya Wanawake.

KAMATI YA UTENDAJI YA BARAZA KUU

6.42 Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa

(b) Makamu wa Mwenyekiti

(c) Katibu Mkuu

(d) Manaibu Katibu Mkuu.

(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake ya Taifa.

(f) Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Taifa.

(g) Wajumbe kumi wa kuchaguliwa na Baraza Kuu.

(h) Mwakilishi mmoja wa Walemavu Taifa ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Wanachama wenye Ulemavu katika ngazi ya Taifa

(i) Mwakilishi mmoja wa Vijana Taifa ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Wanachama Vijana ngazi ya Taifa.

6:43 Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itakutana mara tatu kwa mwaka.

6:44 Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kuweka taratibu kuu za Chama

(b) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Chama

(c) Kuandaa vikao vya Baraza Kuu.

(d) Kupokea na kujadili taarifa ya Wadhamini juu ya hali ya mali za Chama.

(e) Kuajiri Makatibu wa Mikoa na Maafisa Watendaji wa Chama ambao Mamlaka za Ajira zao yapo chini ya Kamati ya Utendaji.

(f) Kusimamia vyombo vya Uchumi vya Chama.

(g) Kuhakikisha kuwa hesabu za Fedha za Chama zinakaguliwa kila mwaka na taarifa zinatolewa kwenye Baraza Kuu.

(h) Kujadili pia mambo yanayowahusu Vijana na Walemavu.

(i) Itakapofika wakati wa Uchaguzi Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itafanya yafuatayo:-

(1) Kupendekeza Vigezo vya kuwapata Viongozi wa Chama.

(2) Kuchagua Wadhamini wa Chama

(j) Bila ya kuathiri kifungu cha 6.44 (i) (2) cha Katiba hii, Wagombea wote watatakiwa kuwa na uzoefu wa uongozi ndani ya Chama usiopungua miaka kumi.

6.44A Kutakuwa na Kamati ya Wanawake ya KUBK ambayo Wajumbe wake watakuwa ni Wajumbe wanawake wa Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu la Taifa.

6.44B Kazi ya Kamati ya Wanawake ya KUBK ni kuweka na kupendekeza masuala yote ya jinsia na maendeleo ya Wanawake kwenye Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu (KUBK).

SURA YA SABA

S. 7 <u>BARAZA LA WADHAMINI</u>

7:0 Baraza la Wadhamini litakuwa na Wadhamini wanne na mmojawao awe Mwanamke.

7:1 Mjumbe wa Baraza la Wadhamini atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) Awe Mfanyakazi mwenye umri wa kuanzia miaka 35 ambaye bado yupo katika Ajira na amekuwa Mwanachama si chini ya miaka 10.

(b) Wawili kati yao wawe wanaishi mahali ambapo si mbali sana na Mji yalipo Makao Makuu ya Chama.

(c) Wawe ni Wanachama wenye heshima, maadili na nidhamu ya hali ya juu.

7:2 (a) Wadhamini wa Chama watachaguliwa na Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu na kuthibitishwa na Baraza Kuu .

(b) Kabla ya kuchaguliwa majina yatatokana na maombi yaliyoombwa kwa kutumia Fomu Maalumu na kupigiwa kura na KUBK.

(c) Wadhamini watafanya kazi chini Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu Taifa

(d) Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itatangaza nafasi iliyo wazi ya Mdhamini.

(e) Nafasi iliyo wazi ya Mdhamini itajazwa na Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu na kuthibitishwa na Baraza Kuu.

7:3 Wadhamini watafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kusimamia Mikataba yote, Hati na Dhamana za Fedha, Viwanja na Mali za Chama zitamilikiwa na kuthibitishwa kwa jina la Baraza la Wadhamini kwa kuzingatia maagizo, maamuzi na maelekezo ya Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu na kuhifadhiwa na Katibu Mkuu.

(b) Mali zote za Chama zinazohamishika na zisizohamishika zitakuwa chini ya uangalizi wa Baraza la Wadhamini wa Chama.

(c) Hundi zote za Chama Makao Makuu lazima ziwe na angalau Saini moja ya Mdhamini

(d) Mdhamini hataruhusiwa kuweka rehani Mali yoyote kwa madhumuni ya kujinufaisha mwenyewe kupitia
Chama hiki.

(e) Wadhamini watatoa taarifa ya kazi zao kwa Katibu Mkuu ambaye ataziwasilisha kwenye Kamati ya
Utendaji ya Baraza Kuu.

(f) Wadhamini watachagua Mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao.

(g) Mwenyekiti na Katibu wake wataalikwa kuhudhuria katika kikao cha Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu pale inapolazimu.

(h) Wadhamini watahudhuria vikao vya Baraza Kuu la Taifa kama waalikwa.

(i) Vikao vya Wadhamini vitafanyika mara mbili kwa mwaka.

7:4 Mwanachama ataacha kuwa Mdhamini iwapo:-

(a) Atafukuzwa Uanachama

(b) Atakuwa hana akili timamu baada ya kuchunguzwa na kuthibitishwa na Daktari bingwa wa maradhi ya akili.

(c) Atavunja maadili ya Chama.

(d) Akitiwa Hatiani na Mahakama na kupatikana na kosa la Jinai.

(e) Atajiuzulu

(f) Atastaafu

(g) Atafariki dunia

(h) Atafikisha umri wa miaka sitini (60).

SURA YA NANE

S. 8 <u>MIGOGORO YA KIKAZI</u>

8:0 Mgogoro wowote utakaotokana na tofauti ya tafsiri ya Kanuni hizi kati ya Chama, Matawi, Kamati zilizochaguliwa, Maafisa waliochaguliwa au Wanachama unaweza kupelekwa katika Kamati ya Utendaji ya Chama.

8:1 (a) Kamati ya Utendaji ya Chama itawajibika kwa maazimio ya jumla yatokanayo na majadiliano na migogoro lakini itakasimu baadhi ya madaraka yake kwa Katibu Mkuu.

(b) Kwa upande wa Majadiliano/Mkataba unaohusu Sekta nzima ya kikazi, lipelekwe kwenye Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu.

(c) Matawi yana haki ya kujitetea dhidi ya Mwajiri na kuendesha shughuli za majadiliano Tawini. Hata hivyo kwa madhumuni ya kuhakikisha mipango mizuri kuhusu Sera za Mishahara, Mikataba ya kwenye Matawi itawasilishwa mbele ya Kamati ya Utendaji kwa uthibitisho kabla ya kutiliana saini.

(d) Ili kurahisisha Makao Makuu ya Chama kusaidia Kuondoa migogoro ya kikazi kabla haijawa mikubwa, Matawi yatawajibika kuleta taarifa za awali juu ya matatizo yanayotarajiwa kuzuka au yakiwa yamezuka kwa Katibu mkuu kwa kupitia Katibu wa Mkoa.

(e) Ili kuzuia migogoro isiyokuwa ya lazima kutokea, ni vema kura ya maoni kuhusu mgomo ipigwe katika kikao cha Wanachama wote wa Tawi. Maoni yatakayotolewa yatasaidia kutia msukumo kwa Mwajiri, hasa kama wengi walipendekeza mgomo. Hali hii inawezekana kumfanya Mwajiri akapata mawazo ya kukubaliana kufikia kwenye usuluhishi. Ili kuhakikisha kuwa mgomo unaotazamiwa unaungwa mkono na wengi, inafaa ielezwe kwamba maoni sharti yakubaliwe na theluthi mbili ili yawe na nguvu.

SURA YA TISA

S. 9 MAPATO YA CHAMA

9:0 Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu inaweza kuchangisha michango maalum, kwa ajili ya Miradi ya Chama baada ya kupata kibali kutoka Baraza Kuu la Taifa.

9:1 (a) Ada ya huduma

(b) Mauzo yatokanayo na mali za Chama

(c) Mapato yatokanayo na Wahisani

(d) Njia nyinginezo za Mapato kama itakavyoamriwa na kukubalika katika vikao.

(e) Mapato yatokanayo na Miradi ya Kiuchumi

(f) Riba itokanayo na Amana za Chama.

9.2 Fedha zitatumika kwa mambo yafuatayo:-

(a) Malipo ya Mishahara, Posho na gharama za Maofisa wa Chama,
(b) Malipo ya Ushirikishwaji wa Chama

(c) Malipo ya gharama za kuendesha Kesi katika kulinda haki za Chama na Wanachama.

(d) Kutatua migogoro ya kikazi

(e) Malipo ya mambo ya Utawala wa Chama, Ukaguzi wa Fedha za Chama.

(f) Uwekezaji kama itakavyoamriwa na Baraza Kuu la Chama la Taifa.

(g) Malipo mengine halali ya Umma yakiwemo Kodi za Serikali na Vikao mbalimbali

(h) Malipo ya adhabu yoyote itolewayo dhidi ya Chama.

(i) Mafunzo mbalimbali ya Wanachama na Watumishi

9:3 (a) Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu itawajibika kwa Baraza Kuu la Taifa katika uendeshaji na usimamizi wa Fedha.

(b) Akaunti zote zitafunguliwa kwa jina la Chama na kuhakikisha Fedha zote zinaingizwa katika Akaunti hizo husika.

(c) Fedha zote zitazopokelewa zitawekwa katika Akaunti ya Chama.

(d) Katibu Mkuu/Katibu wa ngazi husika atafungua Akaunti katika Benki kwa jina la Chama.

9:4 (a) Kamati ya Utendaji ya Mkoa itapitisha Bajeti ya Chama kwa ngazi ya Mkoa.

(b) Baraza Kuu litapitisha Bajeti ya Chama kwa ngazi ya Taifa.

(c) Mapato yatagawanywa kwa Matumizi ya Viwango maalumu kwa ngazi mbalimbali za Chama kama itakavyoamriwa na Baraza Kuu la Taifa.

9:5 (a) Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu Taifa itaamua juu ya manunuzi, usambazaji na Utunzaji wa Mali za Chama kama itakavyoamriwa na Baraza Kuu.

(b) Mali zote za Chama zisizohamishika na zinazohamishika zitakuwa chini ya uangalizi wa Baraza la Wadhamini wa Chama.

9:6 Hesabu za Chama zitakaguliwa mara moja kwa mwaka na Mkaguzi anayekubalika au Mkaguzi mahususi aliyeteuliwa na Baraza Kuu la Chama.

SURA YA KUMI

S. 10 <u>MENGINEYO</u>

10:0 Bila kuathiri yaliyomo katika baadhi ya vifungu vya Katiba hii, kiwango cha mahudhurio kwa mikutano yote ya Chama itakuwa ni zaidi ya nusu ya Wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria mkutano huo.

10:1 Kwa mkutano Mkuu wa dharura au usio wa kawaida kiwango cha mahudhurio ni theluthi mbili ya Wajumbe.

10:2 Kila nafasi itakapoachwa wazi katika Chama mamlaka husika itaijaza nafasi hiyo katika muda usiozidi miezi kumi na mbili (12).

10:3 (a) Mwanachama anayetaka kujitoa kwenye Chama, atafanya hivyo kwa kufuata Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004, kifungu cha 61 (4)

(b) Kiongozi wa Chama anayetaka kujitoa anaweza kufanya hivyo kwa kuandika barua kwa Katibu wa ngazi iliyomchagua, au kama aliteuliwa kwa Katibu wa Mamlaka iliyomteua.

10:4 (a) Kiongozi yeyote wa kuchaguliwa atakayefanya kinyume na maadili ya Katiba ya Chama atasimamishwa Uongozi.

(b) Viongozi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu watasimamishwa Uongozi na Baraza Kuu la Taifa, uamuzi wa kumsimamisha wa Baraza Kuu utakuwa na nguvu na utaanza kazi mara moja mpaka Mkutano Mkuu utakapotoa uamuzi wa mwisho kuhusu tuhuma dhidi ya Kiongozi husika.

(c) Kiongozi aliyechaguliwa ataondolewa na Mamlaka iliyomchagua na atakuwa na haki ya kuomba rufaa katika Mamlaka ya juu inayofuatia.
Bila kuathiri haki hiyo, uamuzi wa Mamlaka iliyomuondoa utaanza kazi mara moja na utakuwa na nguvu mpaka uamuzi wa mamlaka ya juu utakapotoa maamuzi juu ya rufaa yake ambapo uamuzi huo utakuwa ni wa mwisho.

(d) Kiongozi wa kuteuliwa atasimamishwa na Katibu Mkuu na uamuzi wa kumsimamisha utakuwa na nguvu hadi Kamati ya Utendaji au Baraza Kuu itakapotoa uamuzi.

10:5 Ni haki ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) kuitisha Mgomo pale inapobidi.
Kabla ya kuitisha Mgomo Wanachama watatakiwa kupiga kura kuamua Mgomo uitishwe au usiitishwe na kuridhiwa na Baraza kuu la Taifa baaada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu Taifa.
Kanuni za Chama zitatoa utaratibu wa kuendesha kura ya kuamua juu ya Mgomo.

10:6 Nafasi ya Uongozi itahesabiwa kuwa iko wazi endapo Kiongozi anayehusika atakuwa:-
(a) Amekosa Sifa za kuwa kiongozi

(b) Amejiuzulu (Kujitoa)

(c) Hana Akili timamu na kuthibitishwa na Daktari wa maradhi ya Akili

(d) Amefukuzwa Uongozi/ kazi

(e) Amestaafu

(f) Amefariki dunia

(g) Ametimiza umri wa miaka sitini (60)

(h) Amehamishwa Kituo cha Kazi

10:7 (a) Kila Mwanachama hai ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa kuwa Mjumbe katika ngazi yoyote ya Chama (kama hafungwi na Kifungu cha 3:10 (a) – (i).

(b) Bila ya kuathiri kifungu cha 10.7 (a) cha Katiba hii, kila mgombea awe na umri usiozidi miaka 55 wakati wa kugombea

(c) Endapo mtendaji wa Chama mwenye ajira ya kudumu atagombea uongozi katika ngazi ya Kitaifa ya Chama na jina lake likapendekezwa na kamati ya uchaguzi atapewa ruhusa ya maandalizi na kushiriki uchaguzi.

(d) Bila kuathiri kifungu (c) hapo juu, Mtendaji aliyepewa ruhusa ya maandalizi na kushiriki Uchaguzi, katika kipindi cha ruhusa atakuwa nje ya Ofisi na hatatekeleza majukumu yake ya awali ndani ya Chama.

(e) Endapo mtumishi wa Chama mwenye ajira ya kudumu aliyegombea uongozi ngazi ya Taifa na kushindwa kupata kura za kutosheleza kupata nafasi aliyoigombea, ataendelea kuishikilia nafasi yake ya awali ndani ya Chama.

(f) Mtendaji wa Chama mwenye ajira ya kudumu ambaye atagombea na kuchaguliwa kwenye nafasi aliyogombea, atakoma katika nafasi yake ya awali aliyokuwa akitumikia ndani ya Chama kabla ya kuanza kutumikia cheo chake kipya.

(g) Bila kuathiri matakwa ya vifungu (c) - (f), Mtendaji wa Chama ambaye anahudumu nafasi inayopatikana kwa kuchaguliwa, akikosa nafasi anayogombea, hataweza kurejea kwenye nafasi yake ya awali aliyokuwa nayo kabla ya kupata nafasi aliyoipata baada ya kuchaguliwa.

10:8 Uchaguzi utafuata taratibu hizi:-

(a) Mwanachama hai tu ndiye atakaye-hudhuria vikao anavyohusika navyo na kuwa na haki ya kupiga kura.

(b) Kura zote zinazohusu Uchaguzi zitafanywa kwa Siri.

(c) Ikiwa Mgombea ni mmoja mshindi atalazimika kupata zaidi ya nusu ya wapiga kura na iwapo nafasi zinazo- gombewa ni zaidi ya moja washindi watapatikana kwa wingi wa kura.

(d) Watumishi wataruhusiwa tu kupiga kura katika shughuli za Tawi la Wafanyakazi na kwenye Baraza la Wafanyakazi wa Chama.

10:9 Kutakuwa na Tawi la Wafanyakazi, litaitwa Tawi Maalum la Wafanyakazi la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE).

10:10 Kutakuwa na Baraza la Wafanyakazi la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), jukumu lake ni kumshauri mwajiri kuhusu namna ya kuboresha maslahi ya Watumishi na kuongeza Tija Mahala pa Kazi.

10:11 Muda wa Uongozi katika Chama ni miaka mitano, lakini Mjumbe yeyote anaweza kuchaguliwa tena kugombea katika nafasi hiyo au nyingine kwenye Uchaguzi unaofuatia kwa awamu mbili zaidi kama tu hatakuwa amestaafu au kutimiza miaka sitini (60).

10:12 Kikao chochote cha Chama kinaweza kuunda Kamati za kusaidia utekelezaji wa kazi zake. Kamati zitafafanuliwa zaidi kwenye Kanuni za Chama.

10:13 (a) Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake na kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa na theluthi mbili ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu.
Mali yote itakuwa chini ya Wadhamini wa Chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi Nchini.

(b) Maamuzi ya kufuta Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) ni lazima yaelezee mgawanyo wa mali za Chama kama Baraza Kuu na Wadhamini wa Chama watakavyopendekeza kwa kuzingatia Sheria za Nchi.

(c) Uamuzi wa kujiunga na Chama kingine unaweza kuchukuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama ukizingatia maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya hoja, au mapendekezo yanaweza kupigiwa kura na Mkutano Mkuu kama Wajumbe wake watakuwa wamepata taarifa mwezi mmoja kabla ya Mkutano.

10:14 (a) TUGHE haitakuwa na uhusiano wa Kikatiba na Chama chochote cha Siasa. Endapo patahitajika kuwa na uhusiano wa Chama chochote uamuzi utatolewa na Mkutano Mkuu.

(b) Kiongozi yeyote wa TUGHE wa kuchaguliwa au kuteuliwa katika ngazi yoyote hataruhusiwa kuwa Kiongozi katika Chama chochote cha Siasa.

10:15 Mwenyekiti wa Taifa akitoka Sekta ya Serikali Makamu Mwenyekiti atoke Sekta ya Afya au kinyume chake.

10:16 Endapo yatatokea matatizo ama Malalamiko yoyote katika kutafsiri Katiba hii aidha kutokana na kukosekana kwa kipengele na (vifungu) au matatizo mengine, basi Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na uwezo wa kutafsiri katiba hii kulingana na madhumuni yake. Tafsiri sahihi ya mwisho itatolewa na Baraza Kuu la Taifa kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

10:17 (a) Mabadiliko ya Katiba yatafanyika tu pale theluthi mbili (2/3) ya Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wenye haki ya kupiga kura kukubali mabadiliko hayo.

(b) Kanuni za Chama zitawekwa kabla ya kuitishwa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa kwa ajili ya marekebisho ya Katiba.

(c) Mapendekezo au masahihisho; taarifa zake ni lazima ziwe zimemfikia Katibu Mkuu siku sitini (60) kabla ya kufunguliwa kwa Mkutano Mkuu ambao utajadili mapendekezo hayo.

10:18 (a) Kutakuwa na Kanuni za Chama zitakazotafsiri zaidi Katiba na zitakwenda Sambamba na Katiba ya Chama.

(b) Pale ambapo patakuwa na lalamiko au utatanishi Katiba itatawala.

(c) Kanuni za Chama zitatungwa na Baraza Kuu la Taifa. kutokana na mapendekezo ya KUBK.

(d) Kanuni hizo zitaweka Akidi na jinsi ya kutunza Kumbukumbu za mikutano ya Chama.

10:19 (a) Muda wa Kukaimu nafasi ya Uongozi katika Chama utakuwa si zaidi ya miezi kumi na miwili (12).

(b) Pale ambapo nafasi inapokuwa wazi kutokana na Kufariki, Kufukuza, Kuhama, Kujiuzulu au kujitoa Mamlaka husika zitabidi zijaze nafasi hizo kwa kutangaza nafasi wazi.

10:20 Sababu za kufukuzwa:-

(a) Mwanachama pamoja na Kiongozi wa kuteuliwa au wa kuchaguliwa atafukuzwa Uanachama iwapo tu:-

(i) Amethibitika kutumia Katiba ya Chama vibaya.

(ii) Amethibitika kutumia Fedha za Chama kwa ubadhilifu, na kupoteza au kuharibu mali ya Chama. Inapobidi atachukuliwa hatua za Kisheria.

(iii) Amejipatia Uanachama kwa hila, ujanja au udanganyifu.

(iv) Ni Mwanachama wa Chama kingine cha Wafanyakazi.

(v) Ametenda vitendo vinavyo-pingana na Katiba au maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

(vi) Amethibitika kuwa msaliti wa Chama.

(b) Taratibu za kufuatwa kabla ya kufukuzwa Uanachama kama itabidi afukuzwe Uanachama.

(i) Mapendekezo yatatoka kwenye ngazi yake husika, yatapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji Mkoa na yatawasilishwa kwenye Baraza Kuu la Taifa kwa uamuzi.

(ii) Katibu Mkuu atawasiliana na Mwanachama kwa maandishi kuhusu uamuzi.

(iii) Mkutano Mkuu utapewa taarifa tu juu ya Kufukuzwa kwa Mwanachama.

(iv)Akifukuzwa Uanachama amefukuzwa pia Uongozi.

10:21 (i) Chama kitaandaa Kanuni za kuwezesha kuendesha Chama mara inapoonekana kuwa na haja kutokana na mahitaji ya Chama.

(ii) Kanuni hizi zitatayarishwa na Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu na kuridhiwa ama kuthibitishwa na kupitishwa na kikao cha juu ambacho ni Baraza Kuu la Taifa.